

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

**BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA
NISHATI NA MAJI (EWURA CCC)**



**MAONI YA BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA CCC) JUU YA OMBI LA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
MAKAMBAKO LA MAPITIO YA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI KWA KIPINDI CHA MIAKA
MITANO KUANZIA 2026/27–2030/31**

1. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA Consumer Consultative Council - EWURA CCC) linapenda kuwasilisha maoni yake kuhusu ombi la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako (MAKUWASA) la kutaka kuidhinishiwa mapitio ya bei za huduma za maji kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2026/27 hadi 2030/31.

Maoni haya yametokana na mapitio ya nyaraka zilizowasilishwa na MAKUWASA, zikiwemo:

- i. Ombi la Mapitio ya Bei (Tariff Review Application),
 - ii. Mpango Biashara wa miaka mitano 2026/27–2030/31 (Business Plan),
 - iii. Mkataba wa Utendaji (Performance Contract),
 - iv. Muhtasari wa Kikao cha Bodi na Orodha ya Mahudhurio ya Kikao cha Wadau,
 - v. Taarifa za Fedha zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG); na
 - vi. Barua ya Wizara ya Maji ya kutokuwa na pingamizi.
2. Ombi la Mapitio ya Bei pamoja na Mpango wa Biashara wa MAKUWASA vinaonesha mapendekezo ya mabadiliko makubwa ya bei, hususan ongezeko la mwaka wa kwanza wa utekelezaji.

Taarifa zilizomo katika Mpango Biashara zinaonesha kuwa wastani wa bei ya maji unakadiriwa kuongezeka kutoka Shilingi 3,016 kwa mita ya ujazo mwaka 2025/26 hadi Shilingi 4,348 kwa mita ya ujazo mwaka 2026/27, sawa na ongezeko la asilimia 44. Hata hivyo, wastani huo unakadiriwa kushuka hadi Shilingi 2,289 kwa mita ya ujazo mwaka 2027/28, sawa na punguzo la asilimia 47, kabla ya kuongezeka hadi Shilingi 2,534 mwaka 2028/29, Shilingi 2,643 mwaka 2029/30 na Shilingi 2,822 mwaka 2030/31 (Business Plan, Jedwali Na. 27, uk. 48).

Katika Ombi la Mapitio ya Bei, taarifa zinaonesha kuwa mwaka 2026/27 bei ya kundi la majumbani inapendekezwa kuongezeka kutoka Shilingi 1,300 hadi Shilingi 4,541 kwa mita ya ujazo; taasisi na biashara kutoka Shilingi 1,700 hadi Shilingi 5,457; viwanda kutoka Shilingi 2,400 hadi Shilingi 7,704; vituo vya kuchotea maji kutoka Shilingi 1,000 hadi Shilingi 3,210; na ujenzi kutoka Shilingi 3,000 hadi Shilingi 9,631 kwa mita ya ujazo (Tariff Application, Jedwali Na. 1.1, uk. 15).

Baraza linaona kuwa viwango hivyo vya kila kundi vinaonesha kuwa athari kwa bili za watumiaji zinaweza kuwa kubwa kuliko inavyoonekana kwa kuangalia ongezeko la wastani wa asilimia 44 pekee. Kwa hiyo, tathmini ya bei inapaswa kuzingatia si wastani wa bei tu, bali pia ongezeko halisi linalokabili kila kundi la watumiaji na kiwango cha matumizi yao.

Baraza pia linaona kuwa, ongezeko kubwa katika mwaka 2026/27, likifuatiwa na punguzo la wastani wa asilimia 47 mwaka 2027/28, linahitaji maelezo ya kutosha kuhusu vipengele vya gharama na mahitaji ya mapato vinavyosababisha mabadiliko hayo makubwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

Katika mapitio yake ya nyaraka za Mamlaka, Baraza limebaini pia kuwa, Mpango Biashara umejengwa kwa msingi kwamba MAKUWASA itategemea kwa kiasi kikubwa mapato yatokanayo na huduma za maji katika kugharamia shughuli zake. Mpango unaeleza kuwa asilimia 88.1 ya mahitaji ya mapato ya Mpango Biashara yanatarajiwa

kutokana na huduma za maji na huduma zinazohusiana, huku asilimia 11.9 ikitarajiwa kuchangiwa na Serikali kupitia Wizara ya Maji (Business Plan, uk. 24).

Baraza linaona kuwa utegemezi huo unaongeza umuhimu wa kuhakikisha kuwa bei inayopendekezwa ina msingi wa gharama unaoweza kuthibitishwa na kwamba athari yake kwa watumiaji imepimwa kwa uwazi kabla ya kuidhinishwa.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuhusu msingi na uhalali wa viwango vya bei vinavyopendekezwa kwa kila kundi la watumiaji, hususan ongezeko kubwa la mwaka 2026/27;
 - ii. Kuitaka MAKUWASA kuwasilisha uchambuzi wa athari za bei katika bili za watumiaji (Bill Impact Analysis), unaolinganishwa na bei ya sasa kwa viwango mbalimbali vya matumizi, ikiwemo matumizi ya mita za ujazo 5, 10, 15 na 20 kwa mwezi;
 - iii. Kuitaka MAKUWASA kufafanua vipengele vya gharama na mahitaji ya mapato vinavyosababisha wastani wa bei kuongezeka kwa asilimia 44 mwaka 2026/27 na kisha kushuka kwa asilimia 47 mwaka 2027/28; na
 - iv. Kuhakikisha kuwa uamuzi wa bei unazingatia uwezo wa watumiaji kumudu huduma pamoja na maboresho ya huduma yanayotarajiwa kutokana na mapato yatakayokusanywa.
3. Mpango Biashara wa Mamlaka unaonesha kuwa MAKUWASA inatambua kuwa hali ya kiuchumi, ikiwemo mfumuko wa bei, kipato cha kaya na kodi, inaweza kuathiri uwezo na utayari wa watumiaji kulipa bili za maji. Mpango pia unatambua umuhimu wa kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa ni za uhakika na zinazomudu kulipika (Business Plan, uk. 14–15).

Katika mapitio ya nyaraka za Mamlaka, Baraza limebaini kuwa wateja wa majumbani ndio chanzo kikubwa cha mapato ya MAKUWASA. Aidha, taarifa zinaeleza kuwa wateja wa majumbani wanachangia takribani asilimia 93.92 ya mapato ya Mamlaka (Business Plan, Executive Summary, uk. x).

Ni mtazamo wa Baraza kuwa mchango huo mkubwa wa wateja wa majumbani una maana kuwa uwezo wa kaya kumudu bei mpya unapaswa kupewa uzito mkubwa katika kufanya uamuzi wa bei. Hata hivyo, katika nyaraka zilizopitiwa, Baraza halikuona tathmini ya kina ya uwezo wa kaya, hususan zenye kipato cha chini, kuendelea kumudu huduma baada ya mabadiliko ya bei.

Baraza pia halikuona uchambuzi unaoonesha uwiano kati ya gharama za huduma ya maji na mapato ya kaya zinazohudumiwa na MAKUWASA, ambao ungewezesha kutathmini kwa usahihi kiwango cha mzigo wa bili kwa watumiaji.

Pamoja na hayo, Mpango Biashara unaeleza kuwa MAKUWASA inatambua maji kuwa hitaji la msingi na imeweka utaratibu wa kuwasaidia wateja wenye kipato cha chini kuunganishiwa huduma kwa kulipa gharama za kuunganishiwa kwa awamu, kupitia makubaliano kati ya Mamlaka na mteja (Business Plan, uk. 13).

Baraza linatambua umuhimu wa utaratibu huo katika kupunguza kikwazo cha gharama za awali za kuunganishiwa huduma. Hata hivyo, utaratibu huo unahusu zaidi gharama za kuunganishiwa na hauoneshi moja kwa moja namna kaya zenye kipato cha chini zitakavyosaidiwa kuendelea kumudu bili za matumizi ya maji.

Baraza linaona kuwa uchambuzi wa uwezo wa watumiaji kumudu gharama ni muhimu zaidi katika mazingira ambayo Mamlaka inategemea kwa kiasi kikubwa mapato kutoka kwa watumiaji ili kugharamia utekelezaji wa Mpango Biashara wake.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuitaka MAKUWASA kuwasilisha tathmini ya uwezo wa watumiaji kumudu bei inayopendekezwa, ikilenga hasa kaya za kipato cha chini na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu;
- ii. Kujiridhisha kuwa bei itakayoidhinishwa inazingatia uwezo wa kaya, hususan zenye kipato cha chini, kuendelea kumudu huduma ya maji;

- iii. Kujiridhisha kuhusu utaratibu uliowekwa na MAKUWASA wa kutambua na kusaidia wateja wenye kipato cha chini, pamoja na namna utaratibu huo utakavyolinda uwezo wao wa kupata na kuendelea kutumia huduma; na
- iv. Kuhakikisha kuwa ongezeko lolote la bei linaendana na maboresho yanayoonekana na kupimika katika upatikanaji, uhakika na ubora wa huduma kwa watumiaji.

4. Makadirio ya mahitaji ya mapato yaliyowasilishwa katika Mpango Biashara wa MAKUWASA yanaonesha kuwa Mamlaka imejumuisha gharama za uendeshaji na matengenezo, uchakavu wa mali pamoja na marejesho ya uwekezaji (Return on Investment – ROI) katika kukokotoa mapato yanayohitajika kutokana na mauzo ya maji.

Jedwali Na. 27 kwenye Mpango huo linaonesha gharama za uendeshaji na matengenezo zikikadiriwa kuwa takribani Shilingi bilioni 1.932 mwaka 2026/27 na kufikia takribani Shilingi bilioni 3.092 mwaka 2030/31. Gharama za uchakavu wa mali zinakadiriwa kuwa takribani Shilingi milioni 450.905 mwaka 2026/27 na Shilingi milioni 506.931 mwaka 2030/31 (Business Plan, Jedwali Na. 27, uk. 48).

Baraza limebaini pia ongezeko kubwa la marejesho ya uwekezaji (Return on Investment – ROI), kutoka takribani Shilingi milioni 65.396 mwaka 2025/26 hadi Shilingi milioni 730.889 mwaka 2026/27, na kuendelea kuongezeka hadi takribani Shilingi bilioni 2.216 mwaka 2030/31 (Business Plan, Jedwali Na. 27, uk. 48). Kwa kuwa marejesho hayo ni sehemu ya mahitaji ya mapato (Revenue Requirement) yanayotarajiwa kurejeshwa kupitia bei, Baraza linaona ni muhimu msingi wa ukokotoaji wake uthibitishwe.

Hata hivyo, Jedwali hilo halioneshi kwa uwazi thamani ya mali iliyotumika kama msingi wa kukokotoa marejesho hayo, kiwango cha marejesho kilichotumika, pamoja na namna mali mpya na mali zilizofadhiliwa kupitia ruzuku zilivyoshughulikiwa katika ukokotoaji huo. Kwa msingi huo, Baraza linaona ni muhimu EWURA kujiridhisha kuhusu vipengele hivyo kabla ya marejesho hayo kuruhusiwa kuwa sehemu ya gharama zinazorejeshwa kutoka kwa watumiaji kupitia bei.

Kuhusu uchakavu wa mali, Mpango Biashara unaeleza kuwa MAKUWASA hutumia njia ya mstari ulionyooka (straight-line method) katika kukokotoa uchakavu (Business Plan, uk. 25). Hata hivyo, matumizi ya njia hiyo pekee hayatoshi kuthibitisha kiwango cha gharama ya uchakavu kinachopaswa kurejeshwa kupitia bei bila kuhakiki thamani ya mali husika, muda wake wa matumizi, mali mpya zitakazoanza kutumika katika kipindi cha bei na vyanzo vya fedha vilivyotumika kuzipata.

Baraza limebaini pia kuwa Jedwali Na. 27 linaonesha kipengele kinachoitwa “Idle fund from investment” cha takribani Shilingi milioni 730.899 mwaka 2029/30 na Shilingi bilioni 1.121 mwaka 2030/31, ambacho kimejumuishwa katika ukokotoaji wa mahitaji ya mapato kutokana na mauzo ya maji (Business Plan, Jedwali Na. 27, uk. 48).

Hata hivyo, Baraza halikuona katika maelezo yanayoambatana na jedwali hilo ufafanuzi wa kutosha kuhusu maana ya kipengele hicho, chanzo chake, namna kilivyokokotolewa na sababu ya kujitokeza katika miaka hiyo. Kwa kuwa kipengele hicho kina athari katika mahitaji ya mapato na hatimaye bei inayolipwa na watumiaji, Baraza linaona ni muhimu msingi wake ufafanuliwe na kuthibitishwa.

Hivyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kufanya uhakiki wa kina wa mahitaji ya mapato ya MAKUWASA ili kujiridhisha kuwa gharama zote zinazokusudiwa kurejeshwa kupitia bei ni za lazima, zina ufanisi na zinahusiana moja kwa moja na utoaji wa huduma;
- ii. Kujiridhisha kuhusu msingi wa kukokotoa marejesho ya uwekezaji, ikiwemo thamani ya mali iliyotumika, kiwango cha marejesho kilichotumika na mali zinazostahili kujumuishwa katika msingi wa ukokotoaji huo;
- iii. Kuhakikisha kuwa mali zilizofadhiliwa kupitia ruzuku au vyanzo vingine visivyotokana na watumiaji zinashughulikiwa ipasavyo katika kukokotoa uchakavu na marejesho ya uwekezaji ili kuepusha watumiaji kubebeshwa gharama zisizostahili;

- iv. Kuitaka MAKUWASA kuwasilisha mchanganuo wa uchakavu wa mali unaonesha thamani ya mali, muda wa matumizi, nyongeza za mali katika kipindi cha bei na chanzo cha fedha cha mali husika; na
 - v. Kuitaka MAKUWASA kutoa ufafanuzi na mchanganuo wa kipengele cha “Idle fund from investment”, ikiwemo maana yake, chanzo, msingi wa ukokotoaji na athari yake katika mahitaji ya mapato na bei.
5. Makadirio ya gharama za uendeshaji katika Mpango Biashara wa MAKUWASA yanaonesha kuwa gharama hizo zinatarajiwa kuongezeka katika kipindi cha utekelezaji wa bei inayopendekezwa. Gharama za uendeshaji na matengenezo zinazotumika katika ukokotoaji wa bei zinaonekana kuongezeka kutoka takribani Shilingi bilioni 1.932 mwaka 2026/27 hadi Shilingi bilioni 3.092 mwaka 2030/31 (Business Plan, Jedwali Na. 27, uk. 48).

Kwa mujibu wa Mpango Biashara, moja ya gharama muhimu katika kipindi hicho ni matumizi ya umeme kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa maji. Mpango Biashara unaeleza kuwa kusukuma maji kutoka **Isoliwaya Wanging’ombe** kupitia vituo vya kusukuma maji hadi **tanki la Kiumba** kutahitaji matumizi makubwa ya umeme. Gharama hizo zimekadiriwa kuwa takribani Shilingi milioni 420.060 mwaka 2026/27, Shilingi milioni 761.488 mwaka 2027/28, na takribani Shilingi milioni 761.494 kwa mwaka katika miaka ya 2028/29 hadi 2030/31 kwa ajili ya uendeshaji wa pampu na uhifadhi wa vyanzo vya maji (Business Plan, uk. 34).

Baraza linatambua kuwa uzalishaji na usambazaji wa maji kwa kutumia pampu unahitaji matumizi ya umeme na kwamba ongezeko la uzalishaji linaweza kuongeza gharama hizo. Hata hivyo, kwa kuwa gharama za umeme zitarejeshwa kupitia mapato ya Mamlaka na hivyo kuathiri bei inayolipwa na watumiaji, ni muhimu kuhakikisha kuwa makadirio hayo yanaendana na kiasi cha maji kinachotarajiwa kuzalishwa na kusambazwa.

Baraza linaona kuwa tathmini hiyo inapaswa pia kuonesha hatua zinazochukuliwa na MAKUWASA kuongeza ufanisi wa matumizi ya nishati na kupunguza gharama za

kusukuma maji, ili watumiaji wasibebe gharama zinazoweza kupunguzwa kupitia matumizi bora ya mitambo na nishati.

Hivyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kufanya tathmini ya kina ya makadirio ya gharama za uendeshaji ili kujiridhisha kuwa gharama zinazorejeshwa kupitia bei ni za lazima, zina ufanisi na zinaungwa mkono na mahitaji halisi ya utoaji wa huduma;
 - ii. Kujiridhisha kuwa makadirio ya gharama za umeme yanaendana na kiasi cha maji kinachotarajiwa kuzalishwa na kusambazwa katika kila mwaka wa kipindi cha bei;
 - iii. Kuitaka MAKUWASA kuonesha msingi wa makadirio ya gharama za umeme, ikiwemo matumizi yanayotarajiwa ya umeme yanayohusiana na uzalishaji wa maji; na
 - iv. Kujiridhisha kuwa MAKUWASA imeweka hatua madhubuti za kuongeza ufanisi wa matumizi ya nishati na kudhibiti gharama za umeme kabla ya gharama hizo kurejeshwa kwa watumiaji kupitia bei.
6. Viashiria vya kifedha na kiutendaji vya MAKUWASA vinaonesha kutokuwiana kwa baadhi ya taarifa zinazohusu ufanisi wa ukusanyaji wa mapato. Mpango Biashara wa Mamlaka unaeleza katika sehemu ya utendaji wa sasa na wa baadaye kuwa ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ni asilimia 90 na lengo ni asilimia 90 ifikapo Juni 2031 (Business Plan, uk. 12–13). Hata hivyo, maelezo ya viashiria vya kifedha yanaweka lengo la kufikia asilimia 100 ifikapo Juni 2030, wakati Jedwali Na. 34 linaonesha kiwango cha asilimia 101 kwa mwaka 2025/26 na makadirio ya asilimia 85 mwaka 2026/27, asilimia 87 mwaka 2027/28 na asilimia 90 kuanzia mwaka 2028/29 hadi 2030/31 (Business Plan, uk. 58–59).

Baraza linaona kuwa tofauti hizi zinahitaji kufafanuliwa, ikiwemo sababu ya makadirio ya ufanisi wa ukusanyaji kushuka kutoka asilimia 101 mwaka 2025/26 hadi asilimia 85 mwaka 2026/27 wakati bei inapendekezwa kuongezeka. Kiashiria hiki kina athari ya moja kwa moja katika uwezo wa Mamlaka kugharamia shughuli zake bila kuongeza mzigo usio wa lazima kwa watumiaji.

Baraza limebaini pia kuwa muda wa kukusanya madeni ya wateja (Accounts Receivable Collection Period) unakadiriwa kuwa miezi minne mwaka 2026/27, miezi mitatu katika miaka ya 2027/28 hadi 2029/30 na kufikia miezi miwili mwaka 2030/31. Mpango wenyewe unaeleza kuwa kipindi cha mwezi mmoja hadi miwili ndicho kinachochukuliwa kuwa cha kuridhisha (Business Plan, uk. 58–59, Jedwali Na. 34).

Aidha, MAKUWASA imepanga kutumia mita za malipo kabla (prepaid meters) kama moja ya hatua za kupunguza madeni, ikiwemo madeni ya taasisi za Serikali, na ina mpango wa kupata na kufunga mita 150 za malipo kabla (Business Plan, uk. 35).

Baraza linaunga mkono hatua zinazolenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo, linaona kuwa kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa bili na kupunguza madeni ni maeneo ambayo yanaweza kuongeza mapato ya Mamlaka bila kutegemea ongezeko la bei pekee.

Baraza linaona kuwa watumiaji wanaolipa bili zao kwa wakati hawapaswi kubebeshwa kupitia bei gharama zinazotokana na mapato ambayo Mamlaka ingeweza kukusanya kwa kuimarisha mifumo yake ya usimamizi wa madeni na ukusanyaji.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Ijiridhishe kuhusu kiwango sahihi cha sasa na malengo ya ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kutokana na kutokuwiana kwa viwango vya asilimia 90, asilimia 100, asilimia 101 na makadirio ya asilimia 85–90 yaliyoainishwa katika Mpango Biashara;
- ii. Kuhakikisha kuwa MAKUWASA inaweka na kutekeleza malengo yanayopimika ya kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na kupunguza muda wa kukusanya madeni;
- iii. Kuitaka MAKUWASA kuonesha mchanganuo wa madeni ya wateja, ikiwemo madeni ya taasisi za Serikali na wateja wengine, pamoja na hatua na muda uliowekwa kwa ajili ya kuyakusanya; na

iv. Kufuatilia utekelezaji na matokeo ya matumizi ya mita za malipo kabla katika kupunguza madeni na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato.

7. Taarifa zilizomo katika Mpango Biashara na Mkataba wa Utendaji wa MAKUWASA zinaonesha kuwa kupunguza maji yasiyoingiza mapato (Non-Revenue Water - NRW) ni moja ya malengo muhimu ya Mamlaka katika kipindi cha mapitio ya bei.

Kwa mujibu wa makadirio yaliyotumika katika kukokotoa bei, kiwango cha maji yasiyoingiza mapato kinatarajiwa kupungua kutoka asilimia 30 mwaka 2025/26 hadi asilimia 28 mwaka 2026/27, kisha asilimia 26 mwaka 2027/28, asilimia 24 mwaka 2028/29, asilimia 22 mwaka 2029/30 na asilimia 20 mwaka 2030/31 (Business Plan, Jedwali Na. 27, uk. 48).

Mkataba wa Utendaji pia unaonesha kiwango cha awali cha NRW cha asilimia 29.3 na lengo la asilimia 28, jambo linalothibitisha kuwa kupunguza maji yanayopotea ama yasiyoingiza mapato ni sehemu ya majukumu ya kiutendaji ya MAKUWASA katika kipindi kinacholingiliana na Mpango Biashara (Performance Contract, uk. 10–11).

Baraza linaona kuwa kupungua kwa NRW kuna umuhimu wa moja kwa moja kwa watumiaji na uendeleu wa kifedha wa Mamlaka. Kila kiasi cha maji kinachozalishwa lakini kisitozwe bili kutokana na uvujaji, hitilafu za mita au sababu nyingine huongeza gharama ya kila mita ya ujazo inayofanikiwa kuuzwa.

Aidha, makadirio ya bei ya MAKUWASA yanategemea kufikiwa kwa malengo hayo ya kupunguza maji yanayopotea. Kwa hiyo, iwapo kiwango hicho hakitapungua kama kilivyopangwa, kiasi cha maji kinachotowwa bili kinaweza kuwa chini ya makadirio na hivyo kuathiri mapato yaliyotumika kuhalalisha bei.

Baraza linaona kuwa kabla ya sehemu kubwa ya mahitaji ya mapato (Revenue Requirement) kuhamishiwa kwa watumiaji kupitia bei, ni muhimu MAKUWASA kuonesha hatua mahsusi zitakazotekelezwa kupunguza upotevu wa maji na matokeo yanayotarajiwa kutokana na kila hatua.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa bei mpya unaambatana na malengo ya kila mwaka ya kupunguza NRW kutoka asilimia 30 hadi asilimia 20 kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Biashara;
- ii. Kuitaka MAKUWASA kuainisha hatua mahsusi, gharama na muda wa utekelezaji wa shughuli zitakazopunguza upotevu wa maji, pamoja na matokeo yanayotarajiwa;
- iii. Kujiridhisha kuwa makadirio ya kiasi cha maji kitakachotozwa bili na mapato yanayotokana na mauzo ya maji yanaendana na malengo halisi na yanayoweza kutekelezeka ya kupunguza NRW; na
- iv. Kufuatilia utekelezaji wa malengo ya NRW katika kipindi chote cha uhalali wa bei na kuhakikisha kuwa maboresho ya ufanisi wa mfumo yanachangia kupunguza shinikizo la gharama kwa watumiaji.

8. Makadirio ya uzalishaji na mauzo ya maji yaliyotumika katika kukokotoa bei inayopendekezwa yanaonesha kuwa mafanikio ya makadirio ya mapato ya MAKUWASA yanategemea kwa kiasi kikubwa ongezeko la uzalishaji na kiasi cha maji kitakachotozwa bili, hususan kuanzia mwaka 2027/28.

Kwa mujibu wa Mpango Biashara, uzalishaji wa maji unaotumika katika ukokotoaji wa bei unakadiriwa kuwa mita za ujazo 986,230 mwaka 2026/27 na kuongezeka hadi mita za ujazo 2,500,473 mwaka 2027/28. Katika kipindi hicho, kiasi cha maji kinachotarajiwa kutozwa bili kinaongezeka kutoka mita za ujazo 710,086 hadi mita za ujazo 1,850,350. Makadirio yanafikia uzalishaji wa mita za ujazo 2,568,508 na kiasi cha maji kinachotozwa bili cha mita za ujazo 2,054,806 mwaka 2030/31 (Business Plan, Jedwali Na. 27, uk. 48).

Baraza linaona kuwa ongezeko hili ni dhanio (assumption) muhimu katika ukokotoaji wa mapato na bei. Kwa hiyo, ni muhimu kujiridhisha kuwa miundombinu inayotegemewa kuongeza uzalishaji itakuwa imekamiliwa, kujaribiwa na kuanza kutoa huduma kwa wakati unaolingana na makadirio hayo.

Baraza limebaini pia kuwa taarifa za uzalishaji katika sehemu mbalimbali za Mpango wa Biashara zinatumiya viashiria tofauti. Kwa mfano, Mpango unaeleza uzalishaji wa sasa wa takribani mita za ujazo 4,873.24 kwa siku (Business Plan, uk. 17), wakati sehemu ya dhanio/assumption kuu inaeleza uwezo wa uzalishaji unaotarajiwa kuongezeka kutoka mita za ujazo 1,915,885 hadi mita za ujazo 3,492,685 kwa mwaka (Business Plan, uk. 2–3), na Jedwali Na. 27 linatumia makadirio mengine ya uzalishaji katika ukokotoaji wa bei (Business Plan, uk. 48).

Tofauti hizo zinaweza kuwakilisha uzalishaji halisi, uwezo wa uzalishaji au uzalishaji unaotarajiwa. Hata hivyo, kwa kuwa uzalishaji na kiasi cha maji kinachotowza bili ni msingi wa makadirio ya mapato, kila kiashiria kinapaswa kufafanuliwa na kuoanisha kwa uwazi ili kuepusha matumizi ya misingi isiyolingana katika ukokotoaji wa bei.

Aidha, Baraza halikuona uchambuzi wa hali mbadala unaoonesha athari katika mapato, gharama na utekelezaji wa Mpango Biashara iwapo ongezeko la uzalishaji au mauzo ya maji litachelewa au halitafikiwa kwa kiwango kilichokadiriwa.

Kwa maoni ya Baraza, uchambuzi wa hali mbadala (Sensitivity Analysis) ni muhimu ili kubaini uwezo wa MAKUWASA kuendelea kutoa huduma endapo baadhi ya dhanio muhimu zilizotumika kukokotoa bei hazitatekelezeka kama ilivyopangwa.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuhusu uhalisia na uwezekano wa kufikiwa kwa ongezeko la uzalishaji na kiasi cha maji kitakachotowza bili, hususan ongezeko kubwa linalotarajiwa kati ya mwaka 2026/27 na 2027/28;
- ii. Kuitaka MAKUWASA kuoanisha na kufafanua takwimu za uzalishaji halisi, uwezo wa uzalishaji, uzalishaji unaotarajiwa na kiasi cha maji kinachotarajiwa kutowza bili;
- iii. Kujiridhisha kuwa miundombinu inayotegemewa kuongeza uzalishaji itakuwa imekamili na kuanza kutoa huduma kwa wakati unaoendana na makadirio yaliyotumika katika ukokotoaji wa bei; na

iv. Kuitaka MAKUWASA kuwasilisha uchambuzi wa hali mbadala unaoonesha athari katika mapato, gharama, utekelezaji wa miradi na uendelevu wa huduma iwapo uzalishaji, mauzo ya maji au malengo ya NRW yatakuwa chini ya makadirio.

9. Mpango wa Uwekezaji pamoja na makadirio ya gharama za utekelezaji wa Mpango Biashara wa MAKUWASA vinaonesha kuwa Mamlaka imepanga kutekeleza shughuli na uwekezaji wenye thamani kubwa katika kipindi cha miaka mitano.

Kwa mujibu wa Mpango Biashara, gharama ya jumla ya utekelezaji wa Mpango huo ni takribani Shilingi bilioni 33.575, ambapo takribani Shilingi bilioni 19.565 ni matumizi ya uwekezaji (Capital Expenditure - CAPEX) na takribani Shilingi bilioni 13.900 ni gharama za uendeshaji na matengenezo (Operation and Maintenance - O&M) (Business Plan, uk. 47).

Baraza linatambua umuhimu wa MAKUWASA kufanya uwekezaji unaohitajika ili kuongeza uzalishaji, kupanua mtandao, kupunguza upotevu wa maji na kuboresha huduma kwa wananchi. Hata hivyo, ukubwa wa Mpango wa Uwekezaji unahitaji kuendana na uwezo halisi wa Mamlaka kutekeleza miradi kwa wakati na kutumia fedha kama zilivyokusudiwa.

Baraza limebaini kuwa katika kipindi cha Amri ya Bei (Tariff Order) iliyopita, MAKUWASA inaeleza kuwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ulifikia asilimia 80.5 (Tariff Application, Sehemu ya 7.0, uk. 9).

Baraza linaona kiwango hicho kinaonesha kuwa baadhi ya shughuli zilizopangwa katika kipindi kilichopita hazikutekelezwa kikamilifu. Hivyo, kabla ya kuidhinisha mapato mapya kwa ajili ya mpango mkubwa zaidi wa uwekezaji, ni muhimu kujiridhisha kuhusu shughuli ambazo hazikutekelezwa, sababu za kutotekelezwa, fedha zilizokuwa zimetengwa na iwapo shughuli hizo zimehamishiwa katika Mpango Biashara wa 2026/27–2030/31.

Aidha, ni muhimu kuhakikisha kuwa watumiaji hawatozwi tena kupitia bei mpya kwa shughuli ambazo tayari zilikuwa zimegharamiwa au mapato yake yalishakusanywa kupitia bei iliyopita bila kupata huduma iliyokusudiwa.

Kuhusu jambo hili, Baraza linaishauri EWURA mambo yafuatayo:

- i. Kufanya tathmini ya kina ya Mpango wa Uwekezaji wa MAKUWASA ili kujiridhisha kuwa miradi iliyopangwa ni ya lazima, ina vipaumbele vinavyoeleweka na inaweza kutekelezwa katika muda uliopangwa;
- ii. Kuitaka MAKUWASA kuwasilisha mchanganuo wa kila mradi mkubwa unaoonesha gharama, chanzo cha fedha, mwaka wa utekelezaji, hatua iliyofikiwa na manufaa yanayotarajiwa kwa watumiaji;
- iii. Kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa asilimia 80.5 wa shughuli zilizopangwa chini ya Amri ya Bei iliyopita, ikiwemo kubaini shughuli ambazo hazikutekelezwa na sababu zake;
- iv. Kuhakikisha kuwa shughuli ambazo zilifadhiliwa kupitia bei iliyopita hazirejeshwi tena kwa watumiaji kupitia bei mpya bila kufanya upatanisho wa fedha zilizokusanywa na matumizi yaliyofanyika; na
- v. Kuhakikisha kuwa gharama za uwekezaji zinaanza kuathiri bei kwa namna inayolingana na muda ambao miundombinu husika imekamilika na kuanza kutoa manufaa kwa watumiaji.

10. Vyanzo vya fedha vya Mpango Biashara wa MAKUWASA vinaonesha kuwa sehemu kubwa ya gharama za Mpango inatarajiwa kugharamiwa kupitia vyanzo vya ndani vya Mamlaka, huku sehemu nyingine ikitarajiwa kufadhiliwa kupitia ruzuku. Kati ya gharama ya jumla ya takribani Shilingi bilioni 33.575, takribani Shilingi bilioni 22.464 zinatarajiwa kutoka katika vyanzo vya ndani vya Mamlaka, wakati Shilingi bilioni 11.111 zinatarajiwa kutoka katika ruzuku za Serikali (Business Plan, uk. 47).

Mpango pia unaeleza kuwa, bei inayokadiriwa ni muhimu katika kugharamia takribani asilimia 66.9 ya shughuli zilizopangwa, jambo linaloonesha kuwa watumiaji kupitia malipo ya huduma wanatarajiwa kuwa chanzo kikubwa cha fedha za utekelezaji wa Mpango Biashara.

Baraza linaunga mkono upatikanaji wa fedha za Serikali na vyanzo vingine kwa ajili ya kuboresha huduma za maji. Hata hivyo, pale ambapo uwekezaji umefadhiliwa kwa ruzuku, ni muhimu kuhakikisha kuwa gharama hizo hazirejeshwi tena kutoka kwa watumiaji kupitia vipengele vya bei.

Hili ni muhimu zaidi kwa kuwa mahitaji ya mapato ya MAKUWASA yanajumuisha pia uchakavu wa mali na marejesho ya uwekezaji. Bila kutenganisha mali zilizofadhiliwa na watumiaji na zile zilizofadhiliwa kwa ruzuku, kuna hatari ya gharama za uwekezaji huo kuathiri bei zaidi ya mara moja.

Baraza linaona pia kuwa manufaa ya ruzuku za Serikali yanapaswa kuonekana katika kupunguza kiwango cha gharama kinachopaswa kubebwa na watumiaji, badala ya ruzuku kutazamwa kama chanzo cha fedha kisicho na athari katika ukokotoaji wa bei.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuwa kila mradi wa uwekezaji umeainishwa pamoja na chanzo chake cha fedha, ikitenganisha fedha za MAKUWASA na ruzuku;
 - ii. Kuhakikisha kuwa gharama za mali na miradi iliyofadhiliwa kupitia ruzuku hazirejeshwi tena kwa watumiaji kupitia bei kwa namna isiyostahili;
 - iii. Kufanya uhakiki wa namna mali zilizofadhiliwa kupitia ruzuku zilivyoshughulikiwa katika kukokotoa uchakavu wa mali na marejesho ya uwekezaji;
 - iv. Kujiridhisha kuwa mabadiliko yoyote katika upatikanaji wa ruzuku yanazingatiwa katika mahitaji ya mapato na bei, ili watumiaji wasibebe gharama ambazo tayari zimefadhiliwa kupitia chanzo kingine; na
 - v. Kuhakikisha kuwa manufaa ya fedha za Serikali na ruzuku yanaonekana katika upatikanaji wa huduma bora na kupunguza shinikizo la gharama kwa watumiaji.
11. Taarifa za kifedha za kihistoria zilizojumuishwa katika Mpango Biashara zikilinganishwa na Taarifa za Fedha zilizokaguliwa zinaonesha tofauti muhimu zinazohitaji kufanyiwa upatanisho wa takwimu kabla ya taarifa hizo kutumika kama msingi wa kufanya uamuzi wa bei. Kwa mfano, Mpango Biashara unaonesha katika makadirio ya kifedha mapato

ya jumla ya Shilingi 2,021,280,188 kwa mwaka 2023/24 (Business Plan, Jedwali Na. 29, uk. 49) wakati Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa inaonesha mapato ya jumla ya Shilingi 1,547,361,970 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Kiasi cha Shilingi 2,021,280,188 kinachooneshwa katika Mpango Biashara kama cha mwaka 2023/24 kinaonekana katika taarifa iliyokaguliwa kama mapato ya mwaka 2022/23 yaliyorekebishwa (CAG Audit Report, Statement of Financial Performance, uk. 28).

Baraza limebaini hali kama hiyo katika vipengele vinavyounda mapato. Mpango wa Biashara unaonesha Shilingi 871,922,051 na Shilingi 1,149,358,137 katika safu ya mwaka 2023/24, wakati taarifa zilizokaguliwa zinaonesha kiasi hicho katika mwaka 2022/23 uliorekebishwa. Kwa mwaka 2023/24, taarifa iliyokaguliwa inaonesha mapato ya kubadilishana (*exchange revenue*) ya Shilingi 929,423,928 na mapato yasiyo ya kubadilishana (*non-exchange revenue*) ya Shilingi 617,938,042 (Business Plan, uk. 49; CAG Audit Report, uk. 28).

Kwa mtazamo wa Baraza, tofauti hii ni muhimu kwa sababu taarifa za kihistoria hutumika kutathmini mwenendo wa mapato na matumizi na kujenga makadirio ya kipindi kijacho. Iwapo mwaka wa msingi au takwimu za kihistoria hazijawekwa kwa usahihi, makadirio yanayotokana nazo yanaweza kutoa picha isiyo sahihi ya mahitaji ya kifedha ya Mamlaka.

Baraza linaona kuwa taarifa zilizokaguliwa zinapaswa kuwa msingi wa kuthibitisha takwimu za kihistoria zinazotumika katika tathmini ya bei. Pale ambapo Mpango Biashara unatumia takwimu tofauti, tofauti hizo zinapaswa kuelezwa na kufanyiwa upatanisho wa takwimu kwa uwazi.

Hivyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuhusu usahihi wa taarifa zote za kihistoria zilizotumika katika Mpango Biashara na Ombi la Mapitio ya Bei kwa kuzilinganisha na taarifa za fedha zilizokaguliwa;

- ii. Kuitaka MAKUWASA kurekebisha au kufafanua tofauti ya mapato ya mwaka 2023/24 kati ya Shilingi 2.021 bilioni iliyooneshwa katika Mpango wa Biashara na Shilingi 1.547 bilioni iliyooneshwa katika taarifa za fedha zilizokaguliwa;
- iii. Kuitaka MAKUWASA kuwasilisha upatanisho wa takwimu za kihistoria kwa kila mwaka, ukionesha wazi chanzo cha kila takwimu na marekebisho yoyote yaliyofanyika; na
- iv. Kuhakikisha kuwa makadirio ya mapato, matumizi na mahitaji ya mapato yatakayotumika kufanya uamuzi wa bei yanajengwa juu ya taarifa sahihi na zilizothibitishwa.

12. Mapendekezo ya MAKUWASA kuhusu gharama nyingine za huduma pamoja na mpango wake wa kuongeza idadi ya wateja katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango Biashara vinaonesha kuwa MAKUWASA inalenga kuongeza idadi ya wateja kutoka 7,402 hadi 9,852 ifikapo Juni 2031, sambamba na upanuzi wa mtandao wa maji kwa kilomita 69.59. Mamlaka pia imeeleza kuwa kwa wateja wenye kipato cha chini, gharama za kuunganishiwa huduma zinaweza kulipwa kwa awamu kupitia makubaliano kati ya Mamlaka na mteja (Business Plan, uk. 13 na Jedwali Na. 17, uk. 29).

Aidha, Ombi la Mapitio ya Bei linaonesha kuwa ada ya kuunganishiwa upya huduma inapendekezwa kubaki Shilingi 15,000 kwa makundi yote, wakati ada ya kuunganishiwa huduma mpya imeainishwa kuwa asilimia 20 ya gharama ya vifaa (Material Cost) (Tariff Application, Jedwali Na. 1.2 na 1.3, uk. 16).

Baraza linaunga mkono kuwepo kwa utaratibu unaowawezesha wananchi kuunganishiwa huduma, hususan kaya zenye kipato cha chini. Hata hivyo, kwa kuwa ada ya kuunganishiwa huduma mpya imefungamanishwa na asilimia ya gharama ya vifaa, ni muhimu kuwepo kwa uwazi kuhusu orodha ya vifaa, bei zake na msingi wa kukokotoa asilimia hiyo ili mtumiaji aweze kujua mapema kiasi anachotarajiwa kulipa.

Baraza linaona kuwa gharama za kuunganishiwa huduma zinapaswa kuendana pia na lengo la MAKUWASA la kuongeza idadi ya wateja na kupanua huduma katika maeneo ambayo bado hayajahudumiwa vya kutosha. Endapo gharama za kuunganishiwa

zitakuwa kubwa au zisizoeleweka kwa watumiaji, zinaweza kuwa kikwazo katika kufikia malengo hayo.

Hivyo Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuwa vipengele vinavyounda gharama ya vifaa na msingi wa kukokotoa asilimia 20 ya ada ya kuunganishiwa huduma mpya vinaainishwa kwa uwazi na vinaeleweka kwa watumiaji;
- ii. Kuhakikisha kuwa MAKUWASA inakuwa na utaratibu unaoonesha gharama za kawaida za vifaa na kazi zinazohitajika katika uunganishaji wa huduma ili kupunguza uwezekano wa tofauti zisizoelezeka kati ya wateja;
- iii. Kujiridhisha kuwa gharama za kuunganishiwa huduma hazigeuki kuwa kikwazo kwa kaya zenye kipato cha chini na wananchi katika maeneo mapya ya upanuzi wa mtandao; na
- iv. Kufuatilia utekelezaji wa utaratibu wa malipo kwa awamu kwa wateja wenye kipato cha chini na mchango wake katika kuongeza idadi ya wananchi wanaounganishiwa huduma.

13. Malengo ya utoaji wa huduma yaliyoainishwa katika Mpango Biashara wa MAKUWASA yanaonesha kuwa Mamlaka imeweka malengo mbalimbali yanayotarajiwa kufikiwa katika kipindi cha utekelezaji wa bei mpya. MAKUWASA inalenga kupunguza maji yasiyoingiza mapato (maji yanayopotea) kutoka asilimia 30 hadi asilimia 20, kuongeza wastani wa muda wa upatikanaji wa maji kutoka saa 22.45 hadi saa 24 kwa siku, kuongeza idadi ya wateja na kuhakikisha kuwa ubora wa maji unakidhi viwango vinavyotakiwa (Business Plan, uk. 12–13).

Aidha, Mpango unaonesha kuwa, kiwango cha wananchi wanaopata huduma moja kwa moja kinatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 62 hadi asilimia 76 ifikapo Juni 2031, kupitia upanuzi wa mtandao wa maji kwa kilomita 69.59 na uwekezaji mwingine katika mfumo wa maji (Business Plan, uk. 17–18).

Baraza linaona kuwa malengo haya ni muhimu kwa sababu ongezeko la bei linapaswa kuambatana na maboresho yanayoonekana katika huduma zinazopokelewa na

watumiaji. Mafanikio ya bei mpya hayapaswi kupimwa kwa ongezeko la mapato ya Mamlaka pekee, bali pia kwa kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma, uhakika wa maji, ubora wa maji, kupungua kwa upotevu wa maji na kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaohudumiwa.

Aidha, Mkataba wa Utendaji wa MAKUWASA unaweka viashiria vya kupima baadhi ya maeneo hayo, ikiwemo wastani wa muda wa upatikanaji wa maji, maji yasiyoingiza mapato na ubora wa maji. Hivyo, viashiria hivyo vinaweza kutumika kufuatilia utekelezaji wa maboresho ya huduma katika kipindi cha bei (Performance Contract, uk. 10–11).

Baraza linaishauri EWURA mambo yafuatayo:

- i. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa bei mpya unaambatana na malengo ya kila mwaka ya utoaji wa huduma yaliyoainishwa katika Mpango wa Biashara na Mkataba wa Utendaji;
- ii. Kufuatilia kwa karibu mabadiliko katika saa za upatikanaji wa maji, kiwango cha NRW, idadi ya wateja wapya, kiwango cha wananchi wanaopata huduma na ubora wa maji;
- iii. Kujiridhisha kuwa uwekezaji unaofadhiliwa kupitia bei unaonesha manufaa yanayopimika kwa watumiaji ndani ya kipindi kilichopangwa; na
- iv. Kuhakikisha kuwa taarifa za utekelezaji wa viashiria muhimu vya huduma zinawasilishwa kwa EWURA na kutumika katika tathmini ya utekelezaji wa Amri ya Bei katika kipindi chote cha uhalali wake.

14. Taarifa kuhusu ubora wa maji zinaonesha kuwa suala la uzingatiaji wa viwango vya ubora wa maji ni mojawapo ya maeneo ambayo MAKUWASA yenyewe imeyatambua kuwa yanahitaji maboresho. Katika orodha ya masuala ya kimkakati, Mpango Biashara umetaja kutokuzingatiwa kikamilifu kwa viwango vya ubora wa maji na kueleza kuwa kukosekana kwa mtambo wa kutibu maji kunachangia kutokidhi kiwango kinachotakiwa cha ukungu wa maji (turbidity) (Business Plan, Jedwali Na. 19, uk. 30).

Mkataba wa Utendaji unaonesha kiwango cha awali cha uzingatiaji wa ubora wa maji cha asilimia 91.7, huku lengo likiwa kufikia asilimia 100. Mkataba huo pia unaeleza kuwa

kipimo cha ubora wa maji kinatokana na uwiano wa sampuli zinazofaulu vipimo dhidi ya jumla ya sampuli zilizopimwa (Performance Contract, uk. 10 na 16).

Kwa upande wa uhakika wa huduma, Mpango Biashara unaonesha wastani wa sasa wa huduma kuwa saa 22.45 kwa siku, huku lengo likiwa kufikia saa 24 kwa siku (Business Plan, uk. 12–13). Mkataba wa Utendaji unaweka lengo la saa 24 za huduma na kufafanua kuwa muda wa huduma ni saa ambazo mtumiaji anaweza kupata maji kwenye bomba la kaya au kituo cha kuchotea maji, na si muda wa uendeshaji wa mitambo pekee (Performance Contract, uk. 11 na 16).

Baraza linaona kuwa ubora na uhakika wa huduma ni masuala ya msingi kwa watumiaji. Kwa hiyo, pale ambapo watumiaji wanatarajiwa kulipa bei mpya, wanapaswa pia kupata uhakika kuwa maji yanayotolewa yanakidhi viwango vinavyotakiwa na kwamba muda wa huduma unaboreka kwa kiwango kilichoahidiwa.

Kutokana na mtazamo huo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuwa MAKUWASA ina mpango unaotekelezeka wa kufikia uzingatiaji wa asilimia 100 wa viwango vya ubora wa maji;
- ii. Kuitaka MAKUWASA kuwasilisha taarifa za ufuatiliaji wa ubora wa maji, ikionesha idadi ya sampuli zilizopimwa, zilizokidhi viwango, maeneo yaliyobainika kuwa na changamoto na hatua zilizochukuliwa;
- iii. Kufuatilia lengo la kufikisha huduma ya maji hadi wastani wa saa 24 kwa siku na kuhakikisha kuwa kipimo hicho kinaakisi muda halisi ambao watumiaji wanaweza kupata maji; na
- iv. Kuhakikisha kuwa maboresho ya ubora na uhakika wa huduma yanakuwa sehemu ya viashiria vya msingi vya kutathmini mafanikio ya bei mpya.

15. Sehemu mbalimbali za Mpango Biashara wa MAKUWASA zinaonesha kutokuwiana kwa baadhi ya malengo muhimu yanayohusu kiwango cha huduma, idadi ya wateja na mapato yanayotarajiwa. Kwa mfano, kwenye Executive Summary, MAKUWASA inaeleza lengo la kuongeza kiwango cha eneo lenye huduma ya maji (water service coverage) kutoka asilimia 91.01 hadi asilimia 97, na wakati huohuo inaeleza kuongeza

idadi ya watu wanaopata huduma (population served) kutoka asilimia 62 hadi asilimia 76 ifikapo Juni 2031 (Business Plan, Executive Summary, uk. xi).

Sehemu ya Service Coverage Projection inaeleza lengo la kuongeza idadi ya watu wanaopata huduma kutoka asilimia 62 hadi asilimia 76 (Business Plan, uk. 18). Kwa kuwa Executive Summary pia inatumia kiashiria cha asilimia 91.01 hadi asilimia 97, Baraza linaona kuwa maana na msingi wa ukokotoaji wa viashiria hivyo viwili vinapaswa kufafanuliwa kwa uwazi.

Baraza linaona kuwa viashiria hivi vinaweza kuwa na maana tofauti, kwa mfano eneo lenye mtandao wa maji dhidi ya idadi ya watu wanaopata huduma moja kwa moja. Hata hivyo, tofauti hiyo haijafafanuliwa kwa uwazi katika nyaraka, hivyo inaweza kuleta changamoto katika kufuatilia mafanikio ya huduma.

Baraza pia limebaini tofauti katika lengo la idadi ya wateja. Executive Summary na Jedwali Na. 17 vinaonesha lengo la kuongeza wateja kutoka 7,402 hadi 9,852 (Business Plan, Executive Summary, uk. xi; Jedwali Na. 17, uk. 29), wakati Mpango Kazi unaonesha shughuli ya kuongeza idadi ya wateja kutoka 7,402 hadi 9,708 (Business Plan, uk. 35).

Pia, Executive Summary na dhanio kuu za Mpango Biashara zinaonesha lengo la kuongeza makusanyo ya mauzo ya maji kutoka Shilingi 837,070,264 hadi Shilingi 5,211,965,283, wakati Mpango Kazi unaonesha lengo la mapato ya mauzo ya maji la Shilingi 3,369,084,751 ifikapo Juni 2031 (Business Plan, Executive Summary, uk. xi; uk. 2–3; Mpango Kazi, uk. 35).

Kwa maoni ya Baraza, kutokuwiana huku ni muhimu kwa sababu idadi ya wateja, kiwango cha huduma na mapato yanayotarajiwa ni baadhi ya dhanio zinazotumika kutathmini uwezo wa Mamlaka kugharamia shughuli na kuhalalisha bei inayopendekezwa.

Bila kuwepo kwa takwimu moja iliyoidhinishwa na inayotumika kwa sehemu zote za Mpango Biashara na Ombi la Mapitio ya Bei, inakuwa vigumu kufuatilia utekelezaji wa malengo na kutathmini iwapo mapato yanayotarajiwa kupitia bei yanaendana na huduma zitakazotolewa.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuitaka MAKUWASA kuoanisha na kufafanua viashiria vya asilimia 91.01 hadi 97 na asilimia 62 hadi 76, ikieleza maana, msingi wa ukokotoaji na namna kila kiashiria kinavyopimwa;
 - ii. Kuitaka MAKUWASA kuthibitisha lengo sahihi la idadi ya wateja kufikia Juni 2031 kati ya 9,852 na 9,708, na kuhakikisha kuwa takwimu hiyo inatumika kwa uthabiti katika Mpango Biashara, Mpango Kazi na makadirio ya kifedha;
 - iii. Kuitaka MAKUWASA kufafanua tofauti kati ya lengo la mapato la Shilingi bilioni 5.212 na Shilingi bilioni 3.369, pamoja na kuonesha ni takwimu ipi inayotumika katika mfumo wa ukokotoaji wa bei; na
 - iv. Kujiridhisha kuwa maamuzi ya bei yanategemea takwimu na malengo yaliyooanishwa, yanayoweza kupimwa na kufuatiliwa katika kipindi chote cha utekelezaji.
16. Baraza limepitia nyaraka zinazohusu ushirikishwaji wa wadau na kubaini kuwa MAKUWASA imewasilisha Orodha ya Mahudhurio ya Kikao cha Wadau kilichofanyika tarehe 18 Machi 2026 kuhusu mapendekezo ya bei za maji. Hata hivyo, katika nyaraka zilizowasilishwa kwa Baraza, Orodha hiyo ya Mahudhurio haioneshi kwa kina hoja na maoni yaliyotolewa na wadau, majibu ya MAKUWASA wala namna maoni hayo yalivyozingatiwa katika bei iliyowasilishwa (Orodha ya Mahudhurio ya Kikao cha Wadau, tarehe 18 Machi 2026, uk. 1–7).

Baraza linaona kuwa, ushirikishwaji wa wadau katika mchakato wa mapitio ya bei unapaswa kuonesha si tu mahudhurio ya kikao, bali pia taarifa za bei zilizowasilishwa, hoja za watumiaji na wadau wengine, majibu yaliyotolewa na Mamlaka, pamoja na namna maoni hayo yalivyozingatiwa katika maombi ya mwisho ya bei.

Ushahidi huo ni muhimu ili EWURA na wadau waweze kujiridhisha kuwa mchakato wa ushirikishwaji ulikuwa wa maana na uliwawezesha watumiaji kuelewa athari za mapendekezo ya bei na kutoa maoni yao kwa taarifa ya kutosha.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuwa MAKUWASA inawasilisha kumbukumbu kamili ya kikao cha wadau, ikiwemo viwango vya bei vilivyowasilishwa, hoja na maoni ya wadau pamoja na majibu yaliyotolewa na Mamlaka; na
- ii. Kuhakikisha kuwa maoni ya watumiaji na wadau yaliyotolewa katika mchakato wa ushirikishwaji yamezingatiwa ipasavyo katika kufanya uamuzi wa bei.

17. Baada ya kupitia Ombi la Mapitio ya Bei la MAKUWASA pamoja na nyaraka zinazoliunga mkono, Baraza linaishauri EWURA kuzingatia mambo yafuatayo wakati wa kufanya uamuzi kuhusu ombi hilo:

- i. Kujiridhisha kuhusu uhalali wa ongezeko la wastani wa bei kutoka Shilingi 3,016 kwa mita ya ujazo mwaka 2025/26 hadi Shilingi 4,348 kwa mita ya ujazo mwaka 2026/27, sawa na ongezeko la asilimia 44, hususan kwa kuzingatia kuwa wastani huo unakadiriwa kushuka kwa asilimia 47 hadi Shilingi 2,289 kwa mita ya ujazo mwaka 2027/28;
- ii. Kuhakikisha kuwa uamuzi wa bei unazingatia viwango vinavyopendekezwa kwa kila kundi la watumiaji, ikiwemo ongezeko la bei ya majumbani kutoka Shilingi 1,300 hadi Shilingi 4,541 kwa mita ya ujazo mwaka 2026/27, na unaungwa mkono na uchambuzi wa athari katika bili na uwezo wa watumiaji kumudu huduma;
- iii. Kujiridhisha kuwa mahitaji ya mapato yanayotarajiwa kurejeshwa kupitia bei yanahusisha tu gharama ambazo ni za lazima, zina ufanisi na zinahusiana moja kwa moja na utoaji wa huduma, ikiwemo kufanya uhakiki wa gharama za uendeshaji, umeme, uchakavu wa mali na marejesho ya uwekezaji;
- iv. Kuitaka MAKUWASA kufafanua msingi wa kukokotoa marejesho ya uwekezaji yanayoongezeka kutoka takribani Shilingi milioni 730.889 mwaka 2026/27 hadi Shilingi bilioni 2.216 mwaka 2030/31, pamoja na kipengele cha "Idle fund from

investment” kilichojumuishwa katika makadirio ya mahitaji ya mapato (Business Plan, Jedwali Na. 27, uk. 48);

- v. Kujiridhisha kuwa makadirio ya uzalishaji na mauzo ya maji ni halisi na yanaweza kufikiwa, hususan ongezeko la uzalishaji kutoka mita za ujazo 986,230 mwaka 2026/27 hadi mita za ujazo 2,500,473 mwaka 2027/28, pamoja na ongezeko la kiasi cha maji kinachotazwa bili kutoka mita za ujazo 710,086 hadi mita za ujazo 1,850,350 katika kipindi hicho;
- vi. Kuitaka MAKUWASA kuwasilisha uchambuzi wa hali mbadala unaoonesha namna mapato, gharama na utekelezaji wa Mpango wa Biashara vitakavyoathirika iwapo uzalishaji wa maji, mauzo, malengo ya kupunguza maji yasiyoingiza mapato au vyanzo vya fedha havitafikiwa kama ilivyopangwa;
- vii. Kuhakikisha kuwa MAKUWASA inaendelea kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato, kupunguza madeni ya wateja na kupunguza maji yasiyoingiza mapato kabla ya sehemu kubwa ya mahitaji ya kifedha kuhamishiwa kwa watumiaji kupitia ongezeko la bei;
- viii. Kujiridhisha kuhusu kutokuwiana kwa viwango na malengo ya ufanisi wa ukusanyaji wa mapato, ikiwemo asilimia 90, lengo la asilimia 100, kiwango cha asilimia 101 mwaka 2025/26 na makadirio ya asilimia 85–90 katika kipindi cha Mpango (Business Plan, uk. 12–13 na uk. 58–59);
- ix. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa bei mpya unaambatana na malengo yanayopimika ya kupunguza maji yasiyoingiza mapato kutoka asilimia 30 hadi asilimia 20, kuongeza muda wa upatikanaji wa maji hadi saa 24 kwa siku, kuboresha ubora wa maji na kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma;
- x. Kufanya tathmini ya kina ya Mpango wa Uwekezaji wa takribani Shilingi bilioni **19.565** na kuhakikisha kuwa miradi inayofadhiliwa kupitia bei ni ya lazima, ina vipaumbele vinavyoeleweka na inaweza kutekelezwa katika muda uliopangwa (Business Plan, uk. 47);
- xi. Kuhakikisha kuwa miradi iliyofadhiliwa kupitia ruzuku za Serikali haijumuishwi tena katika msingi wa kukokotoa gharama zinazorejeshwa kupitia bei kwa namna itakayoweza kusababisha watumiaji kulipia gharama zilezile zaidi ya mara moja;
- xii. Kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa asilimia 80.5 wa shughuli zilizopangwa chini ya Amri ya Bei iliyopita, ikiwemo kubaini shughuli ambazo hazikutekelezwa,

sababu zake na iwapo shughuli hizo zimehamishiwa katika Mpango mpya wa Uwekezaji;

- xiii. Kuhakikisha kuwa gharama za kuunganishiwa huduma zinaainishwa kwa uwazi, ikiwemo msingi wa asilimia 20 ya gharama ya vifaa kwa huduma mpya, na kwamba gharama hizo hazigeuki kuwa kikwazo kwa kaya zenye kipato cha chini;
- xiv. Kujiridhisha kuhusu usahihi wa taarifa za kihistoria zinazotumika katika makadirio ya kifedha, hususan tofauti kati ya mapato ya mwaka 2023/24 ya Shilingi 2.021 bilioni yaliyooneshwa katika Mpango Biashara na mapato ya mwaka huo ya Shilingi 1.547 bilioni yaliyooneshwa katika taarifa za fedha zilizokaguliwa;
- xv. Kuitaka MAKUWASA kuoanisha takwimu na malengo yanayotofautiana katika nyaraka zake, ikiwemo viashiria vya huduma vya asilimia 91.01–97 dhidi ya asilimia 62–76, lengo la wateja 9,852 dhidi ya 9,708, pamoja na tofauti katika makadirio ya mapato, ili maamuzi ya bei yajengwe juu ya taarifa iliyo wazi na inayoweza kufuatiliwa;
- xvi. Kujiridhisha kuwa ushirikishwaji wa wadau umeandikwa kwa kumbukumbu kamili zinazoonesha viwango vya bei vilivyowasilishwa, hoja za wadau, majibu ya MAKUWASA na namna maoni ya wadau yalivyozingatiwa katika maombi ya bei; na
- xvii. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa bei itakayoidhinishwa unafuatiliwa kwa karibu kupitia taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Biashara na Amri ya Bei, zikiainisha mapato yaliyokusanywa, matumizi yaliyofanyika, hatua ya utekelezaji wa miradi na manufaa yaliyowafikia watumiaji.

18. Baraza linatambua umuhimu wa MAKUWASA kuwa na rasilimali za kutosha ili kuendesha, kutunza na kupanua huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika eneo la Makambako. Baraza pia linatambua malengo ya Mamlaka ya kuongeza uzalishaji wa maji, kupanua mtandao, kupunguza maji yasiyoingiza mapato, kuongeza idadi ya wateja na kuboresha ubora na uhakika wa huduma.

Hata hivyo, kutokana na mapitio ya nyaraka zilizowasilishwa, Baraza linaona kuwa kuna maeneo muhimu yanayohitaji kuhakikiwa na kufafanuliwa kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu bei. Maeneo hayo yanajumuisha ukubwa wa ongezeko la bei kwa

makundi mbalimbali ya watumiaji, mwenendo wa wastani wa bei kutoka mwaka mmoja hadi mwingine, uhalisia wa makadirio ya uzalishaji na mauzo ya maji, mahitaji ya mapato na marejesho ya uwekezaji, matumizi ya ruzuku, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato, utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji, pamoja na kutokuwiana kwa baadhi ya takwimu katika nyaraka za Mamlaka.

Baraza linaona uamuzi wa kuidhinisha bei mpya unapaswa kuzingatia kwa uwiano uendelevu wa kifedha wa MAKUWASA, uhalali na ufanisi wa gharama, uwezo wa watumiaji kumudu huduma na kiwango cha maboresho ya huduma yatakayopatikana kutokana na bei hiyo.

Aidha, Baraza linaona kuwa watumiaji wanapotarajiwa kubeba ongezeko la gharama za huduma, wanapaswa pia kuona maboresho yanayopimika katika muda wa upatikanaji wa maji, ubora wa maji, kupungua kwa maji yasiyoingiza mapato, upanuzi wa huduma na ufanisi wa huduma kwa wateja.

Kwa msingi huo, Baraza linaishauri EWURA kufanya uhakiki wa kina wa maeneo yaliyoainishwa katika maoni haya na kuhakikisha kuwa bei yoyote itakayoidhinishwa inaambatana na masharti yanayopimika ya utendaji, uwazi katika matumizi ya fedha na ufuatiliaji wa karibu wa manufaa yanayowafikia watumiaji katika kipindi chote cha utekelezaji wa bei.

Naomba kuwasilisha.